

Shirika la Wazee la Kaunti ya Milwaukee Zinapatikana kwa wazee wote wenye miaka 60+

Inasimamiwa na Tume inayohusu dira ya Wazee ya kuboresha afya na ustawi kwa wakazi wote wazee wa Kaunti ya Milwaukee kwa kukiri na kushinda ubaguzi wa kimuundo, kukuza usawa wa afya, kuboresha mawasiliano na ushirikiano, na kushughulikia masuala yote ya afya, Shirika la Eneo la Kaunti ya Milwaukee la Wazee:

- Husaidia mtandao mpana, shirikishi, wa huduma za jamii na msaada kwa wazee.
- Huduma za utetezi wa fedha, misaada ya kijamii, usafiri, lishe, afya njema, msaada wa kisheria na walezi kupitia Sheria ya Wazee ya Marekani.
- Huchochea kiwango cha ushiriki katika jamii kupitia Tume ya mabaraza na kamati za Wazee, fursa za kujitolea, na mtandao wa vituo vya wazee.

Kwa pamoja, Kuunda Jamii Maridhawa

Mipango ya Shirika la Eneo la Kaunti ya Milwaukee la Wazee linasaidiwa kwa kiasi fulani na Utawala wa Maisha ya Jamii (ACL), Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani kupitia tuzo za msaada wa kifedha kwa mujibu wa Sheria ya Wazee ya Marekani.

Mpango wa Msaada wa Walezi



MILWAUKEE COUNTY
DEPARTMENT OF HEALTH
& HUMAN SERVICES
**AGING & DISABILITIES
SERVICES**

1220 West Vliet Street, Suite 300 | Milwaukee, WI 53205
(414) 289-6874 | Faksi: (414) 289-8568
county.milwaukee.gov | caregiversuport@milwaukeecountywi.gov



**MILWAUKEE
COUNTY**

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kwa (414) 289-6874

Msaada kwa ajili yako unapowasaidia wengine

Tupo kwa ajili yako kwa kuwa unajali

Je, wewe ni ndugu, mshirika, mwenzi, au rafiki unayemsaidia mpendwa wako kwa kazi za kila siku ili kuhakikisha wako salama, wanajisikia vizuri na wana furaha? Kwa kuwa wewe ni mlezi, tupo ili kukusaidia! Mpango wa Msaada wa Walezi wa Kaunti ya Milwaukee hutoa huduma za msaada, elimu, na utetezi ili kukuza afya na ustawi wa walezi wanapotoa msaada muhimu kwa watu wengine.

Huduma unapozihitaji

- Rasilimali fedha kwa ajili ya walezi kuzitumia ili kujitunza, kupumzika na misaada mingine muhimu
- Ziara za nyumbani na mashauriano ya simu ili kutathmini na kukidhi mahitaji ya mlezi
- Uhusiano wa rasilimali na huduma



Rasilimali fedha kwa ajili ya walezi

Mpango wa Kitaifa wa Msaada kwa Walezi wa Familia

Msaada wa fedha za mafunzo, maboresho ya nyumba, kujitunza, kupumzika, na mahitaji mengine ya mlezi

Nani anaweza kushiriki?

- Walezi wasio rasmi wanaomtunza mtu mwenye umri wa miaka 60 au zaidi au mtu mwenye tatizo la akili wa umri wowote ambaye hajasajiliwa katika mpango wa malezi wa muda mrefu wa Medicaid au anayeishi katika kituo cha malezi.
- Babu/bibi na ndugu wakubwa wenye umri wa miaka 55 au zaidi ambao ni walezi wakuu wa watoto wadogo au mtu mzima mwenye ulemavu.

Mpango wa Msaada wa Familia na Walezi wa Alzheimer

Msaada wa fedha za huduma ya mapumziko kwa mlezi wa muda mfupi, bidhaa au huduma zinazohitajika ili kumtunza mtu mwenye tatizo la akili lisilobadilishika.

Nani anaweza kushiriki?

- Walezi wasio rasmi wanaomtunza mtu wa umri wowote aliyegundulika kuwa na Ugonjwa wa Alzheimer au tatizo jingine la akili pale ambapo mambo yafuatayo yanahusika kwa mtu mwenye tatizo hilo:
 - Anaishi katika mzingira ya jumuiya au ya nyumbani
 - Hajasajiliwa katika mpango wa malezi wa muda mrefu
 - Ana mapato ya mwaka ya \$48,000 au chini yake (ikiwemo mapato ya mwenzi).

SHIRIKA LA ENEO LA KAUNTI YA MILWAUKEE LA WAZEE

ILI KUFAHAMU ZAIDI Piga Simu 414-289-6874 au barua pepe caregiversupport@milwaukeecountywi.gov